

**Swahili transcript:**

Upendo: Ni sehemu nzuri kwa kweli za kwenda kujiburudisha na nini...Na, sehemu nyingine labda ambazo

Happy: Aaah! Sehemu nyingine ni Zanzibar. Lakini Zanzibar ni nzuri, yaani Zanzibar na Bagamoyo unaweza usi..yaani ni sehemu kama mbili ambazo zina...zina uwiano, yaani. Kwa mfano pia ni sehemu ambayo ni ya kihistoria. Kuna historical places nyingi sana Zanzibar.

Upendo: Na kwa Zanzibar kuna historia gani?

Happy: Za watumwa. Kwa mfano waarabu. Kwa mfano ukienda Zanzibar, yaani ukiangalia hata majengo yake yamekaa kama vile yaani majengo Fulani ambayo ni ya kiarabuarabu. Yaani masultani, yaani wake waarabu wale. Ndio maana hata watu wa Zanzibar wenyewe pia wengi wao ni kama waarabuarabu yaani ukiangalia. Kwa hiyo kuna yaani historia za kina Sayyid Said sijui, zote zipo kule Zanzibar unaweza ukaenda. Yaani ni kama vile ina-reflect.

Upendo: Kwa hiyo, ina..inahusisha hii wakati wa biashara ya utumwa; kwamba kulikuwa na soko la watumwa kule Zanzibar.

Happy: Yaah! Ndio maana nasema historia ya Bagamoyo na Zanzibar yaani zina uwiano Fulani kwa sababu zote ni zina mark historia za utumwa, na pia zina historical places nyingi, majengo yake..yaani Zanzibar imekaa kama ni mji vile wa utalii yaani. Ukienda, kuna magofu mengi, majengo yake, milango. Yaani hata ukiangalia milango yake ilivyojengwa,

Upendo: Mmmh!

Happy: Yaani ni ile ni mikubwa, ina paintings nyingi, *so beautiful!* Pia kuna beaches nzuri, hoteli za.

Upendo: Kitalii nzuri

Happy: Mmmh! Kitalii, ukikaa huko, unajiona uko *paradise!*

Upendo: (laughs) OK. Vizuri. Kwa hiyo kwa kweli ni sehemu nzuri sana ya kutembelea; Zanzibar na Bagamoyo na sehemu nyingine. Jiji la Dar Es Salaam unajua ndilo jiji kubwa katika nchi ya Tanzania. Na watalii wengi pia wanakuja Tanzania na watalii wengi wanakuja kutembelea Zanzibar, na kutembelea Bagamoyo, na sehemu nyingine.

**English translation:**

Upendo: Any other places for recreation?

Happy: Another recreational place is Zanzibar. Zanzibar and Bagamoyo are historical and tourist places.

Upendo: What is special in Zanzibar?

Happy: Zanzibar is an historical place that reminds us of the slave trade during the colonial era. Some buildings even look historical. There you can learn about the sultanate Sayyid Said, who was the Arab sultanate in Zanzibar. Most of the people who live there are from that generation of Arabs. They look like Arabs because of intermarriage during the slave trade, when Arabs intermarried with the people of the coast.

Upendo: This reflects the slave trade and the slave market in Zanzibar.

Happy: Yeah! That's why Bagamoyo and Zanzibar have things in common. They share historical events. In Zanzibar, some buildings reflect the colonial era. Even the doors remind one of the colonial Arabs.

Upendo: Mmm!

Happy: They have huge doors with paintings, so beautiful. Also, in Zanzibar, there are many beautiful beaches and tourist hotels. Being there, you feel like you are in Paradise.

Upendo: Okay. So these are nice places to visit: Zanzibar and Bagamoyo, and other beautiful places in Dar es Salaam city. When tourists came to Tanzania, they visit Zanzibar, Bagamoyo and other places.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated